Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**MOSES AMOS MWAKASINDILE**

**DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**045/2019**

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**HUKUMU KUHUSU USTAHILI NA FIDIA**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Mjini Arusha, tarehe 6 Machi 2026:** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ("Mahakama") ilitoa hukumu katika kesi ya *Moses Amos Mwakasindile dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Moses Amos Mwakasindile ("Mwombaji") ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ("Taifa Lililoshtakiwa"). Wakati wa kuwasilisha Ombi hili, Mwombaji alikuwa akitumikia kifungo cha maisha jela baada ya kesi yake kusikilizwa na kupatikana na hatia ya kusafirisha na uuzaji wa dawa za kulevya. Alidai kuwa kulikuwepo na ukiukaji wa haki zake wakati wa kusikilizwa kwa kesi yake mbele ya mahakama za kitaifa.

Taifa Lililoshtakiwa lilipinga kwamba Mahakama haina mamlaka ya kusikiliza kesi zenye madai ya kukiukwa kwa haki za binadamu pamoja na ukubalifu wa Ombi hilo.

Katika pingamizi yake kuhusu mamlaka ya Mahakama ya kusikilizwa kwa kesi zenye madai ya kukiukwa kwa haki za binadamu, Taifa Lililoshtakiwa lilidai kuwa Mwombaji alikuwa anaiomba Mahakama kutathmini ushahidi uliofikishwa mbele ya mahakama zake za kitaifa, na hivyo kuialika Mahakama kutekeleza mamlaka ya rufaa.

Katika kujibu hoja hii, Mahakama ilisema kuwa katika kutekeleza mamlaka yake, kwa mujibu wa Ibara ya 3(1) ya Protokali, haifanyi kazi kama mahakama ya rufaa. Ilidokeza zaidi kwamba haijazuiliwa kuhoji mashtaka yaliyo mbele ya mahakama za kitaifa na kupima utii wao wa Mkataba, Protokali na hati zingine za kimataifa za haki za binadamu

zilizoidhinishwa na Taifa. Katika kesi hii ya sasa, Mahakama ilipata kwamba haki ambazo ilidaiwa kuwa zilikiukwa zinalindwa katika Mkataba ambao Taifa Lililoshtakiwa ni mshirika na hivyo mamlaka ya Mahakama ya kusikiliza kesi zenye madai ya kukiukwa kwa haki za binadamu ilithibitishwa. Pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwa mamlaka ya Mahakama ya kusikiliza kesi zenye madai ya kukiukwa kwa haki za binadamu ilitupiliwa mbali hivyo.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Taifa Lililoshtakiwa, hata hivyo Mahakama ilivichunguza kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya kanuni za Mahakama ("Kanuni"). Kuhusu hilo, Mahakama iliamua kwamba ina mamlaka juu ya watu binafsi kwa kuwa, tarehe 29 Machi 2010, Taifa Lililoshtakiwa liliwasilisha Azimio lililoelezwa katika Ibara ya 34(6) ya Protokali, ambayo inaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi mahakamani dhidi yake kulingana na Ibara ya 5(3) ya Protokali. Mahakama ilisisitiza kwamba kujiondoa kwa Taifa Lililoshtakiwa kwenye Azimio lililotajwa, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Ombi hili kwa sababu kujiondoa kulinza rasmi tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa baada ya Ombi hili kuwasilishwa, tarehe 19 Septemba 2019.

Mahakama pia iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Taifa Lililoshtakiwa kuwa mshirika wa Protokali hii. Mwisho, ilitambua kwamba ilikuwa na mamlaka ya kieneo kwa kuwa matukio yanayozungumziwa yalitokea katika eneo la Taifa Lililoshtakiwa. Kwa hivyo Mahakama iliamua kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Ombi hilo.

Mahakama ilisema kwamba kwa mujibu wa Ibara ya 6(2) ya Protokali, lazima ifanye uamuzi kuhusu ukubalifu wa kesi zote zilizofikishwa mbele yake. Kuhusu Ombi hili la sasa, Taifa Lililoshtakiwa lilitoa pingaizi kuwa Waombaji walikuwa hawajatumia kikamilifu njia zote za usuluhishaji wa ndani. Hususan, Taifa Lililoshtakiwa lilitoa hoja kwamba pamoja na kuwasilisha rufaa katika Mahakama ya Rufaa, Mwasilishaji alistahili kuwasilisha ombi chini ya Ibara ya 30(3) ya Katiba yake na sehemu ya 4 ya Sheria ya Haki za Msingi na Utekelezaji wa Majukumu (BRDEA).

Kuhusu pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa kwa kutotumika kwa njia zote za usuluhishaji za ndani, Mahakama ilisisitiza kuwa katika Ibara ya 56(5) ya Mkataba, ambayo vifungu vyake vinatajwa tena katika Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni hizo, ombi lolote lililowasilishwa mbele yake sharti litimize hitaji la kutumia kikamilifu njia zote za kutafuta suluhisho isipokuwa kama njia hizo hazipo, hazifanyi kazi au hazitoshi au kesi za ndani

zinazozifuata huchukua muda mrefu kukamilika. Kuhusiana na hoja kwamba Mwombaji anastahili kuwa amewasilisha ombi la kikatiba chini ya BRDEA, Mahakama, kwa kurejelea maamuzi yake ya awali, iliamua kwamba suluhisho hili, lililo katika mfumo wa kisheria wa Taifa Lililoshtakiwa, ni suluhisho la kipekee ambalo hakuna mwombaji anahitaji kulitumia kikamilifu. Kwa namna hiyo basi pingamizi ya Taifa Lililoshtakiwa ilitupiliwa mbali.

Huku Mahakama ikiona kuwa hakuna pingamizi iliyotolewa kuhusiana na mahitaji mengine ya ukubalifu, hata hivyo, kulingana na Kanuni ya 50(1) ya Kanuni hizo, ilikagua vigezo vyote vya ukubalifu vilivyotolewa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni hizo, ambayo kimsingi inataja upya vifungu vya Ibara ya 56 ya Mkataba, na kupata kuwa Ombi hilo lilitimiza mahitaji yote.

Kisha Mahakama iliangalia iwapo Taifa Lililoshtakiwa lilikuwa limekiuka Ibara za 2, 4, 6 na 7 za Mkataba.

Kuhusu dai la ukiukaji wa haki ya usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria, Mahakama ilibainisha kuwa wajibu wa kuthibitisha ukiukaji wa haki za binadamu ulikuwa kwa Mwombaji isipokuwa Mahakama iamue vinginevyo. Katika Ombi hili, Mwombaji alidai kuwa haki yake ya usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria vilikiukwa bila kutoa sababu zozote kuthibitisha madai yake. Kwa hiyo, Mahakama ilitupilia mbali dai hili kwa sababu halikuwaza kuthibitishwa.

Kuhusu dai la ukiukaji wa haki ya kuheshimu maisha na uadilifu wa mtu, Mahakama ilianza kwa kukumbusha kwamba haki ya kuishi, chini ya Ibara ya 4 ya Mkataba, haiwezi kukiukwa na itaheshimiwa na haitanyimwa mtu kiholela kwa hali yoyote ile. Mahakama ilisisitiza kuwa wajibu wa kuthinitisha dai la ukiukaji wa haki za binadamu lipo kwenye mtu anyetoa dai hilo. Kwa kuwa Mwombaji alishindwa kutoa sababu au ushahidi wowote kuthibitisha madai yake, Mahakama ilitupilia mbali madai hayo.

Kuhusu madai ya ukiukaji wa haki ya uhuru na usalama wa mtu, Mahakama ilisema kuwa Mkataba unakataza kwa kauli moja kukamatwa na kuwekwa kizuizini kiholela. Ilisisitiza msimamo wake uliojitokeza katika hukumu zake za awali kwamba kukamatwa na kuwekwa kizuizini kunakuwa kwa kiholela ikiwa hakufanyiki kwa mujibu wa sheria, hakuna sababu za wazi na zinazofaa au kunafanywa pasipo na taratibu za ulinzi dhidi ya utekelezaji kiholela. Katika kesi hii, Mahakama ilipata kwamba Mwombaji alikuwa ametoa

dai la kijumla la ukiukwaji wa haki zake chini ya Ibara ya 6 ya Mkataba bila Ushahidi wa kuthibitisha madai hayo. Kwa kuzingatia yaliyosemwa hapo juu, madai yake yalitupiliwa mbali.

Kuhusu dai la ukiukwaji wa haki ya kusikilizwa kwa haki, Mwombaji alitaja namna nne ambazo anaamini kuwa haki yake ilikiukwa. Kwanza, alidai kuwa kizibiti cha dawa za kulevya alichodai kukutwa nacho hakikuorodheshwa kama sehemu ya ushahidi utakaotolewa wakati wa kesi yake. Pili, alidai kuwa msururu wa ulinzi wa vizibiti uliotumiwa dhidi yake ulivunjwa. Tatu, alidai kuwa cheti cha upekuzi na kukamatwa hakikutiwa saini na dereva wa basi la Fuso alimoshikiwa. Nne, alikiri kuwa taarifa ya tahadhari ilichukuliwa nje ya muda wa lazima wa saa nne.

Baada ya kukagua ushahidi wote uliotolewa na Wadaawa, Mahakama iliamua kuwa Mwombaji alikamatwa, kuzuiliwa na hatimaye kufunguliwa mashtaka ya kusafirisha kufanya biashara ya dawa za kulevya za aina ya *Catha edulis*. Kama ilivyoelezwa na Mahakama, idadi ya vifurushi vya *Catha edulis* haikubadilika katika kipindi chote cha kesi hiyo na kwamba hati kadhaa ikiwa ni pamoja na maoni ya kitaalamu kutoka kwa mkemia wa serikali yenye taarifa husika ziliwasilishwa katika Mahakama Kuu. Mahakama pia iligundua kuwa watu wote waliotayarisha hati hizi walihojiwa mahakamani na wakati huu pingamizi zozote kuhusiana na Ushahidi zingetolewa. Hivyo Mahakama iliamua kwamba Mwombaji alishindwa kuthibitisha madai yake.

Kuhusu msururu wa ulinzi wa vizibiti, Mahakama iliamua kwamba, kutokana na uchanganuzi wa ushahidi uliokuwa mbele yake, kwamba hakukuwepo nan a Ushahidi wa kuaminika wa kuunga mkono dai kwamba msururu wa ulinzi ulivunjwa ili kukiuka haki za Mwombaji. Kwa hiyo, dai la Mwombaji lilitupiliwa mbali.

Kuhusu dai kwamba dereva wa basi la Fuso alimokamatwa Mwombaji hakuwa ametia saini cheti cha upekuzi na ukamataji, Mahakama ilisisitiza kwamba watu wote waliosaini cheti cha ukamataji akiwemo Mwombaji, walikuwa nyuma ya gari huku dereva akiwa mbele. Kwa hiyo, madai ya Mwombaji yalitupiliwa mbali.

Mwisho, kuhusu dai la Mwombaji kuwa taarifa yake ya tahadhari ilichukuliwa nje ya muda wa lazima wa saa nne baada ya kukamatwa, Mahakama ilichanganua muda wa matukio na haikupata chochote kuthibitisha kuwa jambo lisilo la haki ilitendwa dhidi ya Mwombaji.

Kwa jumla, basi, Mahakama ilitupilia mbali madai ya Mwombaji ya ukiukwaji wa haki yake ya kesi yake kuendeshwa kwa haki.

Kuhusu fidia, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mwombaji ya kulipwa fidia ikisema kwamba hakuna ukiukwaji wowote uliothibitishwa kutokea ili kumpa Mwombaji haki ya kulipwa fidia.

Kuhusu gharama, Mahakama iliamua kwamba kila mdaawa atajilipia gharama zake.

Kwa mujibu wa Ibara ya 28(7) ya Protokali na Kanuni ya 70 ya Kanuni hizo, Maoni Tofauti ya Jaji Rafaâ BEN ACHOUR na Uamuzi wa Pamoja wa Jaji Blaise TCHIKAYA na Jaji Ntyam O. MENGUE vimeambatishwa kwenye Hukumu hii.

**Kwa taarifa zozote zaidi:**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na matini kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inapatikana katika tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0452019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa baruapepe ifuatayo: registrar@african-court.org

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha kuna ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mahakama hii ina mamlaka juu ya kesi na migogoro yote inayowasilishwa kwake kuhusu ufasiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kwa Haki za Binadamu an Watu na hati zingine zozote muhimu zilizoidhinishwa na Taifa linalohusika. Kwa habari zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu: www.african-court.org